

CIM 316: SPECIAL METHODS IN TEACHING KISWAHILI

MAIN EXAMINATION, 2017/2018.

MAIN CAMPUS

Jibu maswali **MATATU**. Swali la kwanza ni la lazima

Swali la Kwanza

- a) Eleza madhumuni yoyote **MATANO** ya kufundisha Kiswahili katika shule za upili. (Al.10)
- b) Fafanua kwa kinaga ubaga umuhimu wa mpangilio wasomo kwa mwalimu wa Kiswahili katika shule za upili. (Al. 20)

Swali la Pili

- a) Nini maana ya neno "**Sarufi**". (Al. 2)
- b) Imedaiwa kuwa somo la sarufi ni "gumu na kavu". Wewe kama mwalimu wa Kiswahili, eleza hatua utakazotumia katika kufundisha somo la sarufi ili livutie na kuwapendeza wanafunzi. (Al. 18)

Swali la Tatu

- a) Kufaulu kwa somo la Kiswahili sekondari kunategemea uwezo na ubunifu wa mwalimu. Kwa kuzingatia ukweli huu, fafanua sifa zozote **TANO** za mwalimu hodari darasani. (Al. 10)
- b) Eleza vurugu zinazoweza kutokea darasani wakati mwalimu anapofundisha Kiswahili. (Al. 10)

Swali la Nne

- a) Elezamaanaya "**stadi za lugha**". (Al. 2)
- b) Kando na kusoma kimoyomoyo, taja aina nyingine **TATU** za kusoma. (Al. 6)
- c) Bainisha matatizo yoyote **MANNE** ya kusoma kimoyomoyo. (Al. 4)
- d) Jadili dhima ya kusoma kwa ufahamu kwa mwanafunzi wa Kiswahili. (Al. 8)

Swali la Tano

Ushairi ni moja kati ya vipera vya fasihi ya Kiswahili. Wewe kama mwalimu shupavu wa Kiswahili, eleza jinsi utakavyoweza kufundisha somo la ushairi katika shule za upili. (Al.20)